

**UHUSIKA WA SAUTI KAMA MHUSIKA KATIKA
UTEUZI NA UJENZI WA DHAMIRA KATIKA
TAMTHILIA YA KISWAHILI: MFANO WA
TAMTHILIA YA USINIUE (2019) YA ERIC F.
NDUMBARO NA MARIA N. ISAYA**

Furaha J. Masatu

PhD Candidate, The Open University of Tanzania, Tanzania

©2019

**International Academic Journal of Social Sciences and Education (IAJSSE) | ISSN
2518-2412**

Received: 24th July 2019

Accepted: 31st July 2019

Full Length Research

Available Online at:

http://www.iajournals.org/articles/iajsse_si1_39_58.pdf

Citation: Masatu, F. J. (2019). Uhushika wa sauti kama mhusika katika uteuzi na ujenzi wa dhamira katika tamthilia ya kiswahili: Mfano wa tamthilia ya usiniue (2019) ya Eric F. Ndumbaro na Maria N. Isaya. *International Academic Journal of Social Sciences and Education*, 1, 39-58

IKISIRI

Sauti ni mionganini mwa vitu ambavyo ni nadra kuviona vikitumika kama mhusika, aghalabu mhusika mtendaji mwenye nguvu kubwa ya ushawishi na adili kwa jamii kupitia kazi za fasihi andishi, hususani Tamthilia ya Kiswahili. Aina hii ya uhusika na mhusika ni maarufu zaidi katika kazi bunilizi za fasihi simulizi mathalani ngano, visasili na visakale. Kwa fasihi andishi, hasa tamthilia, kazi yenye mhusika Sauti ni pamoja na tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed Khamis, ambayo mhusika Sauti anaonekana kuwa na nguvu kubwa ya ushawishi inayozaa mapinduzi dhidi ya utawala na uongozi dhalimu wa Bi. Kirembwe. Kwa mtalaa huo, makala haya yamechunguza namna mhusika Sauti (katika Tamthilia ya *Usiniue*) alivyoumbiwa nguvu na uwezo wa kutenda na kunena hata kuleta mabadiliko katika jamii kupitia uteuzi na ujenzi wa dhamira.

UTANGULIZI

Makala haya yamegawanyika katika vipengele vikuu vitatu. Kipengele cha kwanza kina vipengele vidogo vitatu vinavyohusika na ufanuzi wa dhana ya mhusika, dhamira na nadharia teule – Ontolojia ya Kiafrika. Kipengele cha pili kina vipengele vidogo vitatu vinavyohusika na wasifu wa waandishi, muhtasari wa tamthilia ya *Usiniue* na ufanuzi juu ya mhusika Sauti. Kipengele cha tatu kinahusika na ubainishaji na mjadala kuhusu dhamira zilizobainika kuzaliwa kutokana na uhusika wa mhusika Sauti. Vipengele hivi vyote vinayajenga makala haya kuwa makala yenye sifa ya kitaaluma kwani mwandishi amerejelea na kuvitambua vyanzo mbalimbali vya maarifa vya kitaaluma kama njia ya kuboresha na kuimarisha andiko. Mwishoni kabisa, mwandishi amefunga makala yake kwa hitimisho kama alivyoanza kwa utangulizi.

Makala yamemtalii kwa kina mhusika Sauti na kubaini ya kwamba, uhusika wake ni wa thamani na umeleta majonzi kwa familia ya Joan, marafiki, ndugu na jamaa. Hivyo, kuifanya tamthilia hii ya *Usiniue* kuwa mionganini mwa tamthilia mpya za kitanzia za Kiswahili zilizotoka mwaka 2019, kama anavyothibitisha Joan kupitia ujumbe alioacha, ambao sehemu yake inasomeka “[...] Nimekosa amani mimi, nikilala mzimu wa mama yangu na kichanga nilichokiu hunililia sana... Naomba mnisamehe na mniombee msamaha kwa Mungu. Mimi Joan, kwa hiari yangu

Uchunguzi umeongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika ambayo pamoja na mambo mengine, inatambua nafasi ya sauti katika kuwakilisha Mungu, miungu, mapepo, majini na wahenga kwa njia ya matamko. Matamko hayo huweza kuwa ya kikorasi (kujirudiarudia kwa wazo au dhana kwa njia ya mwangwi au dhahiri) ama la. Kupitia uhusika wa mhusika Sauti, uchambuzi umebaini ya kwamba nguvu na ushawishi wa mhusika huyu ni mkubwa na umeibua dhamira tano (5) za msingi kabisa, ambazo ni: haki ya watoto kuishi na kulindwa, umuhimu wa utunzaji wa uumbaji wa Mungu, umuhimu wa kuijandaa sasa kwa faida ya maisha ya baada ya kifo, umuhimu na changamoto za sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano na umuhimu wa kufanya tathmini ya kina kabla ya kufanya uamuza.

Mdalo: Dhamira, Wahusika, Usiniue, Sauti, Kikorasi, Eric F. Ndumbaro, Maria N. Isaya

mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeoyote nimeamua kuutoa uhai wangu leo tarehe 29/05/2019 kwa kunywa sumu.”

UFAFANUZI WA DHANA KIMUHTASARI

Dhana ya Mhusika

Wamitila (2010) anatujuza kuwa, “*wahusika ni viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi [...] hutumika kuiwakilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii fulani.*” Naye Madumulla (2009) anafasili dhana ya wahusika kuwa “*ni watu au viumbe katika kazi ya fasihi waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi.*” Fasili hizi mbili haziko mbali na ile ya Njogu na Chimerah (1999) ambao wanasema “*wahusika ni viumbe wa hadithini wanaotokana na mawazo ya mwandishi au msimulizi, na wanaumbwa ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi / msimulizi [...] ni binadamu na wanyama, au binadamu na mazimwi, ama binadamu na pepo wengine, ama binadamu na hata miti.*” Fafanuzi hizi tatu kwa pamoja zinatupatia picha kuu moja, kwamba, kisanaa wahusika ni dhana, kitu, au kiumbe wakiwemo wanyama, ndege, sauti, miungu, mimea na mtu wa kubuni anayepewa wajibu na mwandishi au msanii kumithilisha ubinadamu halisi wa mwanadamu halisi. Aidha, kiusanwaji, wahusika katika kazi bunilizi zisizokuwa za kisitiara, “*huwa ni wahusika halisi wanaoendana kwa karibu sana na maisha ya kila siku kwa sura yao, mavazi yao, lugha yao, na hulka yao kwa jumla. Na kitabia, hawagawiki kwa urahisi katika makundi mawili, bali huwa na tabia mchangamano. Wahusika ni kipengele muhimu cha muundo wa kazi ya fasihi* (Madumulla, ktj.).”

Dhana ya Dhamira

Senkoro (1987) anapoitazama dhana hii (dhamira) anatukumbusha kuchukua tahadhari kutokana na baadhi ya wanataluma kuchanganya kati ya dhana *maudhui* na *dhamira*. Kwa maelezo yake, dhamira ni sehemu mojawapo katika viungo vya maudhui chenye kufungamana na mawazo anayokusudia mwandishi yaifikie jamii. Mtazamo wa Senkoro hautofautiani sana na ule wa wanataluma walio wengi wa Kiswahili, mathalani Madumulla (ktj.) na Wamitila (ktj.). Madumulla (ktj.) anafasili *dhamira* kama “*wazo kuu katika kazi ya fasihi.*” Wamitila (ktj.) anaonekana kutanua fasili ya dhana *dhamira* kwa maneno haya, “[...] ni wazo gani analolikuza au kuliendeleza mwandishi mpaka mwisho [...] lengo au wazo hilo ndilo linajulikana kama dhamira.” Naye Mulokozi (2017) anapoifasili dhana ya *dhamira*, anaiona kama ni “*mawazo, amali, itikadi; “ukweli” na usahihi wa yale yanayosemwa. Pia suala la “hekima” na kutotoka nje ya mipaka ya itikadi na fikira inayokubalika. Kama ilivyo katika fasihi simulizi, “usahihi” unaozungumziwa hapa si ule wa kisayansi tu, bali pia ni ule wa kijamii – kile ambacho jamii inakikubali na kukihamini. Kadhalika, ukubalifu unahuishisha pia suala la mamlaka na tabaka na itikadi zinazofungamana na mambo hayo, [...].*”

Fasili za watalamu hawa watatu, yaani Madumulla, Wamitila na Mulokozi, hazitofautiani sana kimantiki, ila kiupokevu zinaweza kutofautiana. Mathalani, maneno “*wazo kuu*” katika Madumulla yanaweza kusababisha ukakasi mionganoni mwa wasomaji aghalabu wanaofundishwa ya kwamba, dhamira ni jumla ya mambo anayoyawasilisha au kuyajadili mwandishi katika kazi

yake. Na kwamba, dhamira zimegawanyika katika wazo kuu (dhamira kuu) na mawazo mengine (dhamira ndogo ndogo / nyingine). Kwa aliyeutana na mafundisho ya namna hii, bila shaka, asipojiongeza ataishia kusema wazo kuu ndiyo dhamira halafu kile kinachoitwa *dhamira ndogo ndogo* siyo *dhamira* bali kitu kingine kabisa. Nayo kauli “[...] amali, itikadi; “ukweli” na usahihi wa yale yanayosemwa. Pia suala la “hekima” na kutotoka nje ya mipaka ya itikadi na fikira inayokubalika.” inaonekana kukuza mno upana wa goli linaloitwa *dhamira* kiasi cha kutupeleka katika kile alichokwisha kukitahadharisha Senkoro – dhamira na maudhui kwa sababu, itikadi ni kipengele kingine cha maudhui kama ilivyo msimamo, falsafa, propaganda na mtizamo. Kwa hali hii, hatuna budi kuhitimisha kwa kusema, kwa muktadha wa makala haya, *dhamira* itambulike kama *mada au ajenda alizoziaandaa mwandishi kisha kuzituma kwa jamii kupitia kazi bunilizi, ambapo kwa kusomwa au kusikilizwa, jamii ya watu hupata ari, stadi, maarifa, tabia, hadhari na mafunzo.*

Nadharia Teule: Ontolojia ya Kiafrika

Nadharia hii inaangazia masuala ya mifumo ya maisha ya Mwfrika, kifalsafa zaidi hususani uhusiano wa ubinadamu wa Mwfrika na Mungu, miungu na matendo yanayoongoza kanuni na misingi ya uhai, kuishi na kuenenda katika ulimwengu. Nadharia hii inatuaminisha ya kwamba ulimwengu umeumbwa kwa mahusiano kamili kupitia “ghorofa” ya sakafu tatu za makazi (Mulokozi, ktj.). Sakafu ya kwanza ni ile ya juu ambayo inaitwa mbingu, yenyе kukaliwa na Mungu na miungu. Sakafu ya pili ni ile ya katи ambayo inaitwa ardhi au duniani, yenyе kukaliwa na watu, mazimwi, mapepo, majini, misukule na viumbe wengine. Sakafu ya tatu ni ile ya chini ambayo inaitwa kuzimu, yenyе kukaliwa na wahenga almaarufu kwa jina la mizimu. Kumbe basi, Ontolojia ya Kiafrika hufungamana na imani juu ya miviga, miungu, mizimu, Mungu na viumbe wengine wasioonekana lakini wenye nguvu za sihiri zenye kuamua hatima ya maisha na ustawi wa mwanadamu.

Mulokozi (ktj.) anatujuza ya kwamba, nadharia hii inamtambulisha Mwfrika asili kama kiumbe wenye imani thabit, utii na heshima kubwa kwa: (i) wahenga, (ii) uhai wa viumbe visivyo na mawaa, (iii) uzazi ulio endelevu kwani kupitia uzazi ndipo umilele wa vizazi hujengwa na kuunganishwa na Mungu, miungu na wahenga na hatimaye kuvuna baraka. Na kwamba, kutokuzaa au kutoa mimba ni laana na mkosi kwa familia na jamii nzima, ndiyo maana utoaji mimba unapigwa vita mno lakini uzazi mkubwa (kuzaa watoto wengi) haupigwi vita kwani ni ufahari wa hali ya juu katika familia, ukoo na jamii nzima (p'Bitek, 1975). Vilevile, Waafrika kwa asili hutambua na kutii: (iv) ujamiihaji wa kiduara ambao ni mtu huzaliwa-hukua-huzeeka-hufa-hugeuka mzimu-huzaliwa kwa upya, (v) mazingira asili kwani ndio uti wa mgongo wa uhai na muunganiko kati ya maisha ya mwanadamu na Mungu / miungu, na mwanadamu na wahenga pia Mungu / miungu na wahenga; kwa hiyo kuharibu mazingira ni kufitinisha na kuua umilele.

Aidha, (vi) malezi ni jukumu la jamii nzima kwa msaada wa Wahenga na Mungu / miungu, kwa hiyo wanaokiuka maadili ya jamii ni waasi na chukizo kwa Wahenga na Mungu / miungu na malipizi yake huanzia kwa mlengwa kisha kuhamia kwenye familia nzima au jamii nzima endapo hawatatengenza mambo mapema. Kwa hiyo mtu muovu hapaswi kuishi, na akiishi ni

lazima kufanyike maridhiano (utakaso) kati ya mhusika, familia, jamii na wahenga kwa niaba ya Mungu / miungu tofauti na hapo adhabu ni kali na huweza kusambaratisha vizazi. Pia, (vii) maisha ni kuwa katika mduara wa pamoja kama jamii ya familia moja pana yenyewe kuhusisha wahenga, ukoo, marafiki na majirani. Wahenga huishi na kuwatokea watu kupitia maumbile ya watu waliokufa ama walio hai, au kwa njia ya sauti bila mzungumzaji kuonekana kwa macho ya kawaida, ijapokuwa sauti hiyo huweza kujitambulisha yenyewe au kutambulika kwa kufananishwa na mtu anayefahamika - aliyehai au aliyekufa (Mbiti, 1969).

Kwa ufanuzi huu, tunaona uteuzi wa nadharia hii kuongoza uchambuzi ni sahihi kwani sauti kama mhusika ni jambo mojawapo tena muhimu katika Ontolojia ya Kiafrika. Katika nadharia hii, Waafrika wanaamini kuwa Mungu, miungu, wachawi, wahenga, mapepo na majini huweza kumtokea mtu na kuzungumza naye kwa njia ya sauti njozini ama kwa wazi, au kama kiumbe halisi kama ilivyojitekeza katika *Mirathi ya Hatari* (1977), *Janga Sugu la Wazawa* (2002), na *Marimba ya Majaliwa* (2008). Mazungumzo hayo hulenga kuonya, kuelekeza, kutiisha, kuthibitisha uwepo na ushirika wao katika maisha ya familia pana, kupongeza, kuchochea adhabu kwa kumsema mtu kikorasi hadi ajikinai na mwishowe ajiue au atubu maovu yake mbele ya jamii (Lynch na Roberts, 2010), kutaja kwa uchache. Kwa mtalaa huu basi, uchunguzi wa tamthilia ya *Usiniue* chini ya nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika haukuwa mgumu kumtalii mhusika Sauti ili kubaini dhamira zilizojengwa juu yake.

KUHUSU WAANDISHI, TAMTHILIA YA USINIUE NA MHUSIKA SAUTI

Kuhusu Waandishi

Tamthilia ya *Usiniue* imeandikwa na waandishi wawili amba ni Eric F. Ndumbaro na Maria N. Isaya. Eric F. Ndumbaro ni Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge kilichoko Moshi - Kilimanjaro, katika uwanda wa Mlima Kilimanjaro, nchini Tanzania. Ana Shahada ya Sanaa katika Kiswahili (BA. Kiswahili) na Shahada ya Umahiri/Uzamili ya Sanaa katika Kiswahili (MA. Kiswahili – akitamilikia Fasihi) zote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Chuoni anafundisha kozi za Kiswahili - Lugha, Isimu na Fasihi ikiwemo kozi ya Uandishi wa Kubuni. Pia, hufundisha Kiswahili na utamaduni wa Mswahili kwa wageni wanaohitaji kuelewa na kutumia utamaduni, kusoma, kusikiliza na kuzungumza Kiswahili fasaha na sanifu. Aidha, hujishughulisha na kutafsiri maandiko ya Kiswahili kwenda Kiingereza, na Kiingereza kwenda Kiswahili.

Yeye ni mshindi mara mbili wa *Tuze za Ushairi wa Ebrahim Hussein*, mwaka 2014 na 2017. Vilevile ni mtunzi na mwandishi wa kazi bunilizi za kifasihi katika Kiswahili. Kazi zake zilizo sokoni ni *Chini ya Mwembe* (2017, diwani, kwa ushirikiano na mwandishi mwenza – Gloria D. Gonsalves), *Usiniue* (2019, tamthilia, kwa ushirikiano na mwandishi mwenza – Maria N. Isaya) na *Zawadi ya Wino: Barua kwa Watoto* (2019, mkusanyiko wa hadithi fupi, kwa ushirikiano na waandishi wenza – Gloria D. Gonsalves, Justine P. Kakoko, Paskalina Francis na Rehema M. Kawambwa). Kazi zilizo mbioni kutoka ni pamoja na *Ngoma ya Jini na Hadithi Nyingine*, na *Rubani Mtoto na Hadithi Nyingine*.

Eric F. Ndumbaro ni mtawa wa kiume wa Kikatoliki chini ya Shirika la Ndugu Wafransisko Wakapuchini, Provinsia ya Tanzania, tangu mwaka 1997 alipojiunga. Ndani ya shirika na kanisa amewahi kushika nyadhifa zifuatazo: Mkurugenzi wa Miito wa Provinsia ya Tanzania 2014-2016, Mhalmashauri wa Provinsia ya Tanzania (*Provincial Councilor*) tangu 2014 mpaka hivi sasa. Katika maisha ya kawaida, ni mtu mnyenyeketu, mkimya kiasi, mafariji, mtu wa msimamo thabiti usiroyumbishwa kama tawi la mtu mbele ya upemo, mtulivu na msikivu, mcha Mungu, asiye na ubaguzi, mwenye kuchuja mambo kabla ya kuzungumza, kimbilio la wanyonge na wahitaji, mwenye upemo wa juu kuhusu maisha ya ndani na nje ya utawa, mwenye nidhamu na haiba ya uongozi, utawala na usafi. Zaidi sana, hupendelea kujisomea maandiko ya taaluma, stadi na maarifa tofauti tofauti hasa matini za nadharia, ubunilizi, makala za kitaaluma pamoja na maandiko ya kiroho. Hupendelea kutazama filamu hasa filamu za kipelelezi zenyenye mkururo. Chakula anachopenda zaidi ni wali kwa maharagwe. Kifamilia, kwa upande wa baba ambaye sasa ni marehemu, Mzee Fortunatus Heronimus Ndumbaro, yeye ni mtoto wa pili kati ya watoto sita, lakini kwa mama ni mtoto wa kwanza kati ya watoto wanne wa Bibi Faustina Mbonea Mmbuji wa Kijiji cha Gonja, Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania.

Naye Maria N. Isaya, maarufu kwa lakabu ya *sista kidoti* (kutokana na kuwa na kinundu kati ya pua na mdomo wa juu upande wa kushoto) ni mtawa wa kike wa Kikatoliki chini ya Shirika la Dada Wadogo wa Mtakatifu Fransisko wa Asizi, tangu mwaka 2010 alipojiunga nao mpaka sasa. Yeye ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu (mwaka wa mwisho wa masomo yake, 2016 - 2019) wa Shahada ya Kwanza ya Elimu katika Sanaa (BEd - Arts) akisoma masomo ya Kiswahili na Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge kilichoko Moshi - Kilimanjaro, Tanzania. Ni mwandishi chipukizi katika uga wa uandishi bunilizi wa kifasihi, na tamthilia hii ya *Usiniue* ndio kazi yake ya kwanza kuingia sokoni. Aliwahi kufundisha masomo ya Hesabu, Kiingereza, Kiswahili, Historia na Stadi za Kazi katika shule za awali na msingi za Mother Kevin. Vilevile, amewahi kufundisha masomo ya Kiingereza na Kiswahili katika Shule ya Sekondari ya wasichana ya Mtakatifu Clara. Pia, amewahi kufanya kazi ya kuwashudumia watoto wanaotoka katika mazingira magumu katika kituo chao cha kuwasaidia watoto kilichopo mkoani Arusha kinachoitwa “Mama Kevina Feeding Programme.”

Katika maisha ya kawaida, ni mtu mnyenyeketu, mkimya kiasi, mcha Mungu, mrembo mbichi kimvuto aliyeumbwa akaumbika, asiyependa makuu, mtulivu na msikivu, hana ubaguzi, mwenye kuchuja mambo kabla ya kuzungumza, ana huduma ya udiakonia kwa watoto na wahitaji wengine, ana nidhamu ya juu na haiba ya usafi. Anapendelea kujisomea maandiko ya taaluma, stadi na maarifa tofauti tofauti hasa vitabu vya kiroho na vitabu vingine vya uhamasishaji. Hupendelea sana filamu za Kifilipino. Ni mdau wa mazoezi ya viungo hasa kuruka kamba. Chakula anachopenda zaidi ni wali kwa samaki. Kifamilia, ni mtoto wa nne kati ya watoto watano, ambapo wa kiume ni wanne na wa kike ni yeze peke yake. Wazazi wake ni Mzee Isaya Mohamed na Bibi Florentina Pius Mchomvu wa Kijiji cha Njoro, Wilaya ya Same, Mkoani Kilimanjaro, Tanzania.

Kuhusu Tamthilia ya Usiniue

Usiniue ni tamthilia ya kisasa iliyoandikwa mnamo mwaka 2019 na watanzi chipukizi katika uga wa Fasihi ya Kiswahili, hususani Tamthilia ya Kiswahili. Tamthilia hii inaonesha namna ujana unavyoweza kuwageuka vijana wabichi hasa mabinti hata kusababisha kuzimwa kabisa kwa ndoto zao. Joan, mhusika mkuu, mwanafunzi wa elimu ya juu, anajiingiza katika mapenzi na ngono zembe na hatimaye anapata mimba asiyoitarajia. Mbaya zaidi, anajikuta amepotezana na kijana (Alex) aliyempa ujauzito. Hofu ya kuonekana amesaliti malezi na nasaha za wazazi wake, kwa kudhania ya kwamba Alex alikuwa anamtumia kama chombo cha starehe, hivyo amemkimbia; inamsukuma kwa Sikitu, mwanafunzi mwenzake, ambaye anamshauri na kumsaidia kupata daktari wa kuitoa mimba husika, kwa madai kwamba ujauzito kwa mwanafunzi kijana ni kutaka kujizeesha, kama tunavyomnukuu Sikitu; “*nilitaka nikushangae [...] kujizeesha mapema hivyo [...]*” badala yake inampasa “*Kula kwanza raha [...], kuzaa sahizi ni mapema sana.*”

Pamoja na Joan kusikiliza kisha kutekeleza ushauri wa Sikitu, vita ya nafsini mwake inamkabili na kumzidi nguvu, hatimaye anaamua kujiua kwa kunywa sumu baada ya kugundua ya kuwa Alex hakupotea hewani na machoni kwa bahati mbaya, lakini alijikuta anakosa amani kwa sababu daima majuto ni mjukuu na wema hushinda uovu hata kama ni kwa kuchelewa. Haya yanathibitika kupitia kauli za Joan, mathalani “*Kumbe ninamfikiria Alex wa watu vibaya tu, hivi akija nitamwambia nini kuhusu damu yake? Sipo tayari kuyasema haya kwa kinywa changu. Laiti kama ningalimsikiliza Mary [...].*” Mbaya zaidi, amani ikamkimbia baada ya mizimu kuanza kumuandama mfululizo, kama asemavyo yeze mwenyewe kupitia sehemu ya ujumbe aliuacha baada ya kujiua. Sehemu ya ujumbe inasema, “[...] Nimekosa amani mimi, nikilala mzimu wa mama yangu na kichanga nilichokiuia hunililia sana... Naomba mnisamehe na mniombee msamaha kwa Mungu. Mimi Joan, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nimeamua kuutoa uhai wangu leo tarehe 29/05/2019 kwa kunywa sumu.”

Kuhusu Mhusika Sauti

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) inafafanua sauti kama “*mlio unaotokana na mgongano wa vitu k. v. chuma, msuguano wa ala za kinywa au mwili au kiumbe.*” Lakini pia dhana ya sauti kwa mujibu wa kamusi hii inaweza kutumiwa kurejelea hali au kitendo cha “*kukubaliana na jambo kwa pamoja*” (kwa mfano, *walisema kwa sauti moja*), au ni hali ya “*kuwa na uwezo au madaraka kuhusu jambo fulani*” (kwa mfano, *usikubali kudhalilika hivi hivi. Lazima uwe na sauti na wote watambue u nani kwao*). Kifasihi, hususani katika tamthilia ya *Usiniue* na *Kivuli Kinaishi*, sauti haisimami kama dhana ya mlio, kitendo au hali bali kama mhusika au wahusika wenye kauli moja kimaadili na kimamlaka dhidi ya watu wema au wanaokwenda kinyume na maadili ya jamii. Matumizi ya Sauti kama mhusika bunilizi ni mhusika na mbinu kongwe zaidi katika kazi bunilizi za Fasihi Simulizi za Kiafrika zenye kubeba mithiolojia ya kimazingara (Lynch na Roberts, ktj.; Bertoncini, 1989), lakini mhusika huyu hajitokezi sana katika kazi bunilizi za Fasihi Andishi ya Kiswahili.

Katika tamthilia ya *Usiniue*, ujenzi wa mhusika Sauti una changamoto ya kiufundi inayooonekana wazi. Katika ukurasa wa viii unaobeba orodha na wasifu wa wahusika, kunaoneka hakuna mhusika anayeitwa Sauti badala yake kuna wahusika walioorodheshwa kwa pamoja na kutambulishwa hivi “*Sauti I, II, III: Malaika, Vumilia na Kichanga alichokiuwa Joan.*” Kupitia nukuu hii, mhusika Sauti ni mmoja katika nafsi tatu bila shaka; maana kama ni wahusika watatu tofauti, kiufundi waandishi walitakiwa kuwatofauti hivi: Sauti I: Kichanga alichokiuwa Joan, Sauti II: Mzimu wa Vumilia - mama mzazi wa Joan, Sauti III: Malaika. Hata hivyo, majina haya ya wahusika (Sauti I, II, III) hayaonekani kabisa ndani ya mchezo husika kwa sababu, tunaposoma tamthilia yenyewe tunakutana na mhusika anayeitwa Sauti (uk. 1, uk. 2 na uk. 75) na wahusika Sauti 1, Sauti 2, na Sauti 3 (uk. 73). Kitaaluma na kiufundi, utambulisho wa mhusika kuanzia jina na wasifu wake haupaswi kuwa tofauti, isipokuwa pale tu jamii inapombatiza mhusika jina mbadala kwa sababu maalumu.

Kwa hiyo wahusika Sauti I, II, III na wahusika Sauti 1, Sauti 2, na Sauti 3 ni wahusika tofauti kabisa kama ilivyo kwa mhusika Sauti. Changamoto hii ya kiufundi inakwenda mbali zaidi ambapo Sauti kama mhusika anaonekana kuwa na utambulisho wa namna mbili tofauti ambazo kiufundi hauendani kabisa. Kauli za mhusika Sauti katika ukurasa wa 1 hadi 2 zinathibitisha kwamba ndiye mhusika Sauti 3 wa ukurasa wa 73. Kauli ya mhusika Sauti wa ukurasa wa 75 inatuonesha ni Alex. Aidha, kidini, maneno aliyopewa mhusika Sauti (au Sauti 3) hayapaswi kuwa ni maneno ya malaika bali Mungu. Kama waandishi walikusudia kumtumia Malaika kufikisha ujumbe kutoka kwa Mungu, basi walitakiwa kila mwisho wa tamko waingize maneno haya “asema Mungu” au “asema Muumba wako,” “asema Neno,” au “asema Bwana wa Majeshi” kama walivyofanya manabii katika maandiko matakatifu pindi walipopeleka ujumbe halisi wa Mungu kwa wanadamu; kwa sababu maneno yote ya mhusika Sauti (kama Malaika – uk. viii, uk. 1, uk. 2 na uk. 75) yanaonesha ya kwamba yeze (Sauti/Sauti III/Sauti 3) ndiye muumba wakati kidini siyo kweli; muumbaji ni Mungu (rejea Mwanzo 1 na Mwanzo 2 katika *Maandiko Matakatifu ya Mungu Yaitwayo BIBLIA*).

Pamoja na changamoto hizi za kiufundi, bado hatushindwi kuchunguza namna kauli za mhusika anayetambulika kwa jina la Sauti zinavyoibua dhamira tofauti tofauti. Kwa mtalaa huu, changamoto tulizozitambua na kuzifafanua hapo awali hazitaathiri ubainishaji wa dhamira zilizoteuliwa na kujengwa katika tamthilia ya *Usiniue*. kwa jumla, ujenzi wa mhusika huyu / hawa unaonesha kuwakilisha uwepo wa mamlaka ya kiungu inayochukizwa pia kutoa adhabu kali kwa mtu anayekiuka desturi za kulinda na kutunza misingi ya mnyororo wa uungu - ubinadamu – uhai- ulinzi – maisha.

DHAMIRA ZINAZOIBULIWA NA MHUSIKA SAUTI KATIKA TAMTHILIA YA USINIUE

Haki za Watoto Kuishi na Kulindwa

Haki ya mtoto zinalindwa kisheria kupitia katiba za nchi mathalani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mikataba ya kimataifa na sheria mbalimbali. Kwa

mujibu wa Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara (2016) na Wazambi na Mikongoti (2018), mtoto analindwa pia na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989 ambao Tanzania iliuridhia mnamo Julai 10, 1991; Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990 ambao kwa Tanzania ulisaini Oktoba 3, 1998 na kuridhiwa Machi 16, 2003; Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, Sheria Mpya ya Kazi Na. 6 ya Mwaka 2004, na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. Kwa Tanzania, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 inamfasili mtoto kama “*mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane.*” Akiwemo “*mtoto yatima, mtoto aliye katika mazingira magumu, mtoto aliye zaliwa nje ya ndoa, mtoto wa kuasiliwa, na mtoto anayealelewa katika vituo vya kulelea watoto.*”

Sheria ya mtoto inampa mtoto haki zifuatazo: haki ya kuishi, haki ya kupumzika, haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa, haki ya kutokubaguliwa, haki ya jina na utaifa, haki ya kuishi na wazazi wake, haki ya kupata huduma bora za elimu, malazi matibabu kwa ajili ya ustawi wake, haki ya kushiriki michezo na shughuli za kiutamaduni, haki ya huduma za pekee kwa walemavu, haki ya kunufaika na kutumia kwa uangalifu mali za wazazi wake, haki ya kutoa maoni, mawazo kusikilizwa na kutoa maamuzi ya ustawi wake, haki ya kutokuajiriwa katika ajira zenye madhara, na haki ya kulindwa dhidi ya udhalilishwaji, kijinsia. Miongoni mwa haki hizi ni haki ya kuishi na haki ya kulindwa. Kwa mantiki hii, hata mtoto aliye tumboni naye ni mtoto mwenye haki ya kuishi pia kulindwa na wazazi, jamii lakini zaidi sana kisheria. Katika tamthilia ya *Usinie*, kilio cha mtoto kupewa haki ya kuishi na kulindwa inaonekana kubebwa na kusisitizwa na Mhusika Sauti 1 na Sauti 2 baada ya kuona haki hii ikichezewa kikatili. Sauti 1 na Sauti 2 wanalalama:

- Sauti 1: Kwani mama, nilikukosea nini lakini? Kwa nini uliamua kuniua na kunitupa chooni kama kinyesi? Hata baada ya kukusihi kuwa ‘**usinie**’ kamwe hukutaka kunisikiliza. Kwa nini Joan? Kosa langu ni lipi?
- Sauti 2: Joani mwanangu, kwanini umeniulia mjukuu wangu? Umechagua kuwa mama wa marehemu? (uk. 73)

Sauti 1 anawakilisha watoto waliokatiliwa vikali haki yao ya kuishi na kulindwa, ilhali Sauti 2 anawakilisha jamii ya watu wema wenyewe kumuona mtoto kama zao la jamii, ikiwa ni sehemu ya wajibu wa jamii katika kumlinda mtoto. Sheria ya Mtoto (ktj.) inasema hivi kuhusu wajibu wa jamii kwa mtoto, “*mtu yeyote hapaswi kumbagua mtoto kwa kuzingatia jinsi, utaifa, umri, dini, lugha, siasa, ulemavu, afya, desturi, uzawa, mazingira aliyokulia, kiuchumi, kuwa mkimbizi na mengineyo; Mtu yeyote hapaswi kumnyima mtoto haki ya jina, uraia na haki ya kuwajua wazazi wake wa kumzaa na ndugu zake; Mtu yeyote hapaswi kumnyima mtoto haki ya kuishi na wazazi wake, walezi au familia na kukua katika mazingira salama na ya amani.*” Nukuu hii zinathibitisha ya kwamba wahusika Sauti 1 na Sauti 2 hawajakurupuka kudai haki ya mtoto kuishi na kulindwa bali ni utekelezaji wa mikataba, sheria na kanuni za nchi na zile za kimataifa.

Tatizo la wanawake hususani mabinti kuwanyang’anya watoto haki yao ya kuishi na kulindwa linaonekana kuwa kubwa kadri siku zinavyoongezeka, kama inavyobainishwa katika Mwongozo

wa Stadi za Mpango wa Maisha Tanzania (hakuna mwaka), unaotamka bayana kwamba “*Kukatisha mimba kinyume na sheria (wakati mwingine huitwa “utoaji mimba uchochoroni”)* hufanyika sana kuliko hata watu wengi wanavyojua. Hatari za kiafya ni pamoja na vifo vyatia mzazi na ugumba. Hatari za kihisia na kimwili ni nyingi na msichana huyo anakuwa na uwezekano mdogo wa kuwa alishauriwa kabla na baada ya tukio hilo.” Taarifa hii inapata nguvu pale tunapoibusisha na ripoti za Shirika la Afya Duniani (WHO) ambalo nalo halikubaliani na utoaji mimba usiozingatia miongozo ya sekta ya afya. Ripoti kadhaa za WHO (katika BBC, 19 Januari 2012) zinaonesha ya kwamba; “*kiwango cha utoaji mimba duniani kimebakia kuwa asilimia 28 kwa kila wanawake 1,000. Hata hivyo uwiano wa mimba zinazotolewa bila utaalamu kimepanda kutoka 44% mwaka 1995 hadi 49% mwaka 2008.*” Na kwamba, “*takwimu hizo [...] zinaendelea kuthibitisha kile kinachofahamika kwa miongo mingi kuwa wanawake wanaotaka kutoa mimba wasizozitaka watafuta utoaji huo kwa gharama yoyote hata kama ni kinyume cha sheria au inahatarisha maisha yao.*”

Ndiyo maana, Dr. Richard Horton (BBC, ktj.) anaonekana kuumizwa na kasi ya utoaji mimba pale asemapo, “*Takwimu hizi za sasa zinasikitisha sana. Hatua iliyopigwa miaka ya 1990 sasa ni kinyume [...]*” ikiwa ni muendelezo wa hofu juu ya mwenendo wa mwanadamu dhidi ya ulinzi wa mtoto aliye tumboni mwa mama yake. Kwa Afrika, mathalani Tanzania, ulinzi wa mtoto, hasa aliye tumboni mwa mama yake unamgusa hata mwajiri kwa mfanyakazi wake. Kupitia Sheria Mpya ya Kazi Na. 6 ya Mwaka 2004 (katika Kituo cha Ushauri Nasaha, Lishe na Afya (COUNSENUTH) na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, 2015) mwajiri anashurutishwa kufanya hivi kwa mfanyakazi mjamzito: “*Mwajiri haruhusiwi kumpa mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha kazi ambazo zinahatarisha afya yake au ya mtoto. Endapo mama alikuwa anafanya kazi ambayo inaweza kusababisha hatari kwake au kwa mtoto; mwajiri anapaswa kumpatia kazi mbadala bila ya kukiuka mkataba au makubaliano ya ajira yake. Inapobidi mwanamke kubadilishiwa kazi kutokana na hali ya uzazi.*”

Ripoti ya programu ya DHS (2010) inaonesha kiwango cha juu cha ongezeko la idadi ya mimba za utotonii mionganii mwa wasichana wa Tanzania bara kuliko visiwani. Rika hili ni rika la Joan (anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 19 – 20, Ndumbaro na Isaya, 2019) ambalo pamoja na ukweli kuwa Sheria ya Watoto haiwahesabu kuwa watoto, lakini wengi wao ni dhahiri wangali masomoni, hivyo bado hawajaweza kujitetea wala kukabiliana na changamoto za uzazi na maisha. Jambo hili la kubeba mimba katika umri kama wa Joan, kwa binti ambaye yuko chini ya malezi ya wazazi, kwa sehemu kubwa huchangia sana vitendo vyatia mabinti kuondoa kikatili haki ya mtoto kuishi na kulindwa ili kukwepa lawama, kufukuzwa shule au, na nyumbani, kukimbiwa na wapenzi wao, pia kutengwa kanisani / msikitini kwa kunyanyapaliwa kama watenda dhambi. Hali hii ndiyo iliyomkuta Joan, baada ya Sauti 1, Sauti 2 na Sauti 3 walipoungana kupiga kelele za kumsuta na kumsimanga kikorasi ikiwa ni ishara ya kupinga vitendo vyatia hujuma dhidi ya uhai wa viumbe wema wasio na sauti wala nguvu ya kujitetea hapa duniani.

Kwa hiyo basi, kwa jumla, wahusika Sauti 1 na Sauti 2 wamefanya kazi kubwa ya kuwakumbusha wanawake na jamii nzima juu ya umuhimu wa kulinda na kutetea haki za watoto ili wapate kufurahia zawadi ya uhai waliokirimiwa na Mungu kwani tatizo la utoaji mimba linaonekana kuwa kubwa kadri siku zinavyozidi kusonga mbele. Kwa Wanaontolojia ya Kiafrika, bila shaka wanaweza kusema kwa ujasiri kuwa, matatizo yanayoikumba jamii ya leo, kwa namna moja ama nyingine ni matokeo ya laana na mikosi inayotokana na utoaji mimba, ambao ni kinyume na Mungu, miungu na wahenga (Mbiti, ktj.).

Umuhimu wa Utunzaji wa Uumbaji wa Mungu

Uumbaji wa Mungu ni jambo linalopiganiwa kwa hali na mali na watu wengi. Waandishi wameamua kuingia katika jumuia pana ya wanaharakati wanaotetea haki na maadili ya kuheshimu na kutunza kila kilichoumbwa na Mungu. Dunia ya leo inaonekana kukosa utu, upendo, amani, furaha, busara, hekima, huruma na mapenzi kwa uumbaji wa Mungu. Watu wengi hawajali tena wala kufikiria hatima ya maisha ya vizazi vya jana, leo na vijavyo dhidi ya uharibifu wa uumbaji wa Mungu wanaoufanya sasa (Tumerithi Tuwarithishe, 2016). Haya yanathibitika kupitia nukuu zifuatazo;

Sauti: (*sauti inaendelea kunamba*) Nalikufundisha kukaa na kusimama ukiwa ndani ya tumbo la mamayo. Kuna mwingine awezaye kufanya hivyo? [...] (Bado sauti haijamwacha) Ulipokuwa tayari, niliamrisha malaika kuwa wakati wa ujio wako umewadia. Ulizaliwa pasi na meno ya kula, mikono iso nguvu wala miguu isoweza kutafuta chakula. Nikalainisha mishipa miwili ya kifua cha mamayo ili upate maziwa. Wakati wa msimu wa masika maziwa yalikuwa na joto, na wakati wa msimu wa kiangazi maziwa yalikuwa baridi. (uk. 1)

Sauti 3: Bado sijamaliza! (*sauti inaendelea kusisitiza*). Niliweka mapenzi kwa wazazi wako, hawakula chakula mpaka wewe ushibe, hawakulala mpaka wewe ulale. Je, kwa kuwa sasa una nguvu ndo unaniasi na kunifanyia madhila? Huoni haya kwa uliyoyafanya? Damu ya kiumbe ulichokiuia inanillilia... (uk. 73-74)

Nukuu hizi zinaonesha namna mhusika Sauti / Sauti 3 anavyosimama kidete kutukumbusha hasira na majonzi anayoyapata Mungu pindi tunapoharibu uumbaji alioufanya kwa faida yetu na ya kwake. Ingawa nukuu hizi zinarejelea uumbaji wa binadamu tumboni mwa mama yake, lakini kimawanda zinawakilisha aina zote za uumbaji aliofanya Mungu na kumkabidhi mwanadamu ili autumie na kuutunza kwa busara, nidhamu, maarifa, stadi na uendelevu (Joseph na Bontrager, 2014). Katika zama hizi, dunia imejikuta iko katikati ya hujuma nyingi na za kila aina zinazotishia afya na ustawi wa vyote alivyoviumbaji Mungu. Huku si tu kwenda kinyume na Mungu, bali pia ni kuisigina na kuihujumu Ontolojia ya Kiafrika. Baadhi ya hujuma hizo ni pamoja na: uharibifu wa mazingira unaosababisha kupotea kwa uoto wa asili; ongezeko la hewa ya ukaa duniani; ongezeko la joto duniani; ubaba wa chakula; vifo na kupotea kwa maliasili; kutoweka kwa amani na upendo alioumba Mungu kwa sababu ya ubinagsi, chokochoko na tamaa

za kisiasa, kiuchumi na kijamii mionganoni mwa za jamii watu wa duniani; na uharibifu wa amali - asili za kielimu na kitabibu alizoziumba Mungu.

Mengine ni uharibifu wa teknolojia na sayansi rafiki kwa uhai na afya ya dunia; uharibifu wa ndoa, jinsia na uzazi aliouumba Mungu kutokana na sasa dunia kutaka mimba zitolewe hovyo, wanawake na wanaume wawe na hadhi sawa kimapenzi, kingono na wajibu mwngine; jamii kutokuona umuhimu wa kuzaa, kuijaza nchi, kuitunza na kuitisha nchi kwa namna ambayo kila kitu kilikuwa chema kama alivyoagiza Mungu muumba wa mbingu na nchi (Mwanzo 1: 28 – 31 katika *Bible Society of Tanzania*, 1997). Ndiyo maana katika haya yote, Jochen Motte (hakuna mwaka) anatukumbusha na kutuhamasisha kuunganisha nguvu katika kutunza urithi tuliokabidhiwa kwa faida ya vizazi vya leo na vijavyo kwani hali ni tete mno. Tunamnukuu:

“Muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, mchana na usiku havitakoma” (Mwanzo 8:22). Kufuatana na ahadi hii ya Mungu, Umoja wa Makanisa ya Kiinjili (UEM) tangu 2008, umekuwa ukielimisha makanisa yake kwa njia ya maonyesho na miradi mbalimbali ikihamasisha kwamba, si jukumu la mwanadamu kuiharibu dunia. Mungu ametoa dunia hii kwa wanadamu kama mahali pa kuishi na inapaswa kutunzwa. Leo, mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira ni tishio kubwa kwa wanadamu na kwa mazingira. Makanisa ndani ya UEM katika Afrika, Asia na Ujerumani yameitikia changamoto hii kwa kuweka mikakati katika kukabiliana na mabadiliko haya katika miradi mbalimbali ya mazingira, uelimishaji na uhamasishaji. UEM inajumuika pamoja na makanisa ulimwenguni kote, katika mpango wa “Amani Duniani”. Kwa njia ya kutembeleana, wajumbe [...] wanatiana nguvu katika kupiga vita dhidi ya uharibifu wa misitu, uporaji wa ardhi na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchimbaji wa madini, ulimaji mkubwa wa michikichi, pamoja na uchafuzi wa mazingira mijini.

Matendo haya yote yanatendwa na wanadamu na yamethibitishwa kutendwa na yanaendelea kutendwa. Ushahidi wa hoja yetu unapatikana katika ripoti tofauti tofauti za hali ya uchumi, afya, mazingira, ukimbizi, amani, haki na sheria, dini, ndoa na kadhalika. Mfano wa ripoti hizo ni ripoti za mwaka za Shirika la Mazingira Duniani (UN Environment) za 2016, 2017, 2018, 2019 na zile za The Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC) ambazo kwa pamoja zinathibitisha namna mwanadamu aliyekabidhiwa kutumia na kutunza uumbaji wa Mungu, alivyogeuka laana na tishio kwa kila kiumbe – hadi uhai wake mwenyewe. Ripoti hizi zinaonesha hatari kubwa ya kuwapo tishio baya la afya bora na endelevu kwa dunia na viumbwe vyake. Kumbe basi, Sauti akiwa mhusika anaibua dhamira ya umuhimu wa kutunza uumbaji wa Mungu tuliokabidhiwa kwani Mungu aliumba vitu vyote na kuviona kuwa vi vyema kabisa. Kinyume chake, tutaendelea kuvuna laana na mikosi isiyoisha kupitia magonjwa yasiyo na tiba wala kinga, ushoga, usagaji, ulawiti, vita, vifo visivyo vya kawaida, ukimbizi, ukatili, ukame, uhaba wa maji na chakula, kutaja machache; ikiwa ni sehemu ya machukizo ambayo hayakbaliki hata kwa mapokeo ya Kiafrika.

Umuhimu wa Kujiandaa Sasa kwa Faida ya Maisha baada ya Kifo

Zipo falsafa na nadharia zinazolitazama suala la maisha ya binadamu na hatima yake baada ya kuaga dunia. Wapo wanaoamini ya kwamba, mwisho wa mwanadamu ni kifo na baada ya kufa hakuna jipya linalomtokea zaidi ya kuoza na kuteketea kabisa. Lakini wapo wanaoamini ya kwamba, baada ya kufa kuna uhai tena, na kwamba kipo kipindi cha mpito cha utakaso au adhabu za kungojea hukumu ya Mungu. Kundi hili la pili, linaamini kuwapo kwa hukumu ya mwisho; hata hivyo limegawanyika kuhusu hatima ya mahali awapo mwanadamu pindi angojeapo hiyo hukumu ya mwisho - punde tu roho inapoacha mwili. Kwa Wanaontolojia ya Kiafrika, mwanadamu huoza nyama na mifupa lakini roho yake haifi wala kupotea bali huzaliwa katika umbo jipya. Tamthilia ya *Usiniue* inampa wajibu mhusika Sauti kutukumbusha ya kwamba, kaburini kuna dhiki na kiza, huku tathmini ya yote uliyotenda ukiwa hai itaendelea kufanyika ili kuamua adhabu stahiki. Mhusika Sauti anatukumbusha hivi:

Sauti: Kumbuka hili mwanangu, ulipozaliwa hukujua nani alikutoa kutoka kwa tumbo la mamayo, ukifa hutajua nani atakuweka kaburini. Ulipozaliwa ulioshwa na kusafishwa, ukifa pia utaoshwa na kusafishwa. Ulipokuwa tumboni mwa mamayo ulikuwa kwenye dhiki na kiza. Kadhalika, haburini utakuwa kwenye dhiki na kiza. Basi upeapo kiumbo na kifikra utaulizwa na watu shahada za masomo na ujuzi wako. Ukifa, malaika watakuuliza amali yako na ulivyojiandaa na akhera (*sauti inasisitiza*). (uk. 1)

Funzo tunalolipata hapa ni kwamba maisha ya mwanadamu si kitu si chochote, tulikuja bila kitu tena hatujiwezi na tutaondoka bila kitu tena hatujiwezi. Kwa hiyo mhusika Sauti anatutahadharisha kuwa viumbe watiifu, wanyenyeketu na wenye kuitazama jana yetu ili kuiamua leo yetu kwa faida ya kesho yetu isiyojulikana. Kumbe basi, pamoja na mbwembwe zote za kusaka mali, maarifa, heshima na fahari bado kuna siku itafika tutaviacha vyote na kurudi kusikojulikana tena tukiwa tunasitiwa na tusiowajua kama ilivyokuwa katika nyakati za utoto wa giza totoro. Waandishi kupitia Sauti wanatukumbusha ile falsafa ya Kezilahabi ya kila kiumbe kuzaliwa ili kifanye fujo zake kisha kiondoke na kuwaachia wengine uwanja wa kufanya fujo kwa wakati na utashi wao (Senkoro, 1995).

Hivyo, hatuna budi kutenda mema na kuwa watu wa toba daima kwa sababu kuzaliwa na kufa kwetu hakutofautiani kwani "*ulipozaliwa hukujua nani alikutoa kutoka kwa tumbo la mamayo, ukifa hutajua nani atakuweka kaburini. Ulipozaliwa ulioshwa na kusafishwa, ukifa pia utaoshwa na kusafishwa.*" Hakika hili ni jambo zito lenye fumbo lililojaa giza lisilofumbuka mionganii mwa wanadamu walio hali waliozaliwa na mwanamke mwanadamu kwa kuwa "*Ulipokuwa tumboni mwa mamayo ulikuwa kwenye dhiki na kiza. Kadhalika, haburini (bila shaka ni kaburini – mtazamo wa mwandishi) utakuwa kwenye dhiki na kiza. Basi upeapo kiumbo na kifikra utaulizwa na watu shahada za masomo na ujuzi wako. Ukifa, malaika watakuuliza amali yako na ulivyojiandaa na akhera.*"

Umuhimu na Changamoto za Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mawasiliano ni jambo nyeti sana linalogusa maisha ya kila mtu. Mawasiliano yasipokuwa na maana wala mtiririko chanya muda wote, daima huzalisha kutokuaminiana, kutokuelewana na hatimaye hasara kubwa kwa mtu mmoja mmoja na jamii nzima. Mojawapo ya nyenzo za mawasiliano ni rununu. Pamoja na rununu kuwa njia bora na rahisi katika kuyabeba na kuyafikisha mawasiliano kwa haraka na kwa gharama nafuu mionganoni mwa watu wa zama hizi, hususani katika Afrika, bado teknolojia hii inakabiliwa na changamoto ya kutokupatikana kwa mtandao katika baadhi ya maeneo kutokana na aina ya teknolojia iliyotumika kutengeneza simu husika, wizi wa simu, nishati ya umeme, kiwango cha umasikini wa wakazi, usalama wa mali na teknolojia, populesheni ya watu, jografia ya maeneo, na uwezo wa mitambo ya simu (Rumanyika, 2016). Hali hii ikijitokeza husababisha wafanyabiashara kupata hasara, watu kufanya maamuzi mbadala baada ya kutokukupata, ndoa na mapenzi kuyumba kutokana na wapenzi / wenzi kutokuaminiana kwa hisia ya kuzimiwa simu ili usaliti uweze kutendeka bila bughudha, na kadhalika. Changamoto hii katika mawasiliano chanya imechangia Joan kuchukua uamuzi wa kutoa mimba baada ya Alex “kupotea” hewani na machoni. Tunanukuu:

Sauti: Mpenzi wako Alex. Unaendeleaje Waridi wangu?

Joan: (*Anapigwa na butwaa, haamini anachokisikia, anapumua kwa nguvu, anapiga moyoconde, anajaribu kuficha masaibu yake, kisha anajibu*).
Mhuu...! Wow...! Alex my love, uko wapi mpenzi? Nimekukumbuka sana

Alex: Mhh...! Mbona umepumua hivyo? Nisamehe Waridi wangu, nilipata matatizo makubwa na kupoteza mawasiliano. Leo ndo nimebahatika kuipata namba yako. Vipi kichanga chetu ndo kinakutia hasira hivyo. Hicho lazima kiwe kidume. Nipo njiani nakuja Dar kuwaona wapenzi wangu.

Joan: Mhuuu...! (*anashusha pumzi kwa nguvu kisha anakata simu*). Kumbe ninamfikiria Alex wa watu vibaya tu, hivi akija nitamwambia nini kuhusu damu yake? Sipo tayari kuyasema haya kwa kinywa changu. Laiti kama ningalimsikiliza Mary..., hakika Sikitu ameniingiza choo cha kiume! (*anawaza*) Aha, halafu leo Shangazi Linda na mama walihidi kunipigia simu, nasikitika kwa kuwa hawatanipata, ngoja niharakishe (*anaendelea kuwaza*). (uk. 75)

Mazungumzo kati ya Alex na Joan yanathibitisha athari ya kutokutunzwa kwa mawasiliano kwa njia tofauti tofauti, mfano kuandika kwenye shajara, kuwa na namba za watu wa karibu na mhusika, kuwatambua watu tofauti tofauti wa karibu na mhusika ikiwa ni njia ya kuishi kama familia moja pana yenye kuwasiliana na kutegemeana. Zaidi sana, pana umuhimu wa kuwa watulivu lakini wepesi katika kutafuta mawasiliano mbadala ili kuepuka athari hasi zitokanazo na ukosefu wa mawasiliano chanya, kwa sababu hali ya mawasiliano ya simu katika maeneo ya mashambani bado ni changamoto kubwa (Tanzania Communication Regulatory Authority

(TCRA), Bangladesh Institute of ICT in Development (BIID) and Tanzania Telecentre Network (TTN), 2011). Joan anaonekana kujutia uamuzi uliosababishwa na kitendo cha Alex “kumtelekeza” bila taarifa yoyote kutokana na kutokupatikana hewani kwa kipindi chote tangu walipotengana baada ya Alex kwenda kwao. Bila shaka, Joan alihisi Alex amemkimbia na kubadilisha mawasiliano kama wafanyavyo baadhi ya “wapenzi” hasa vijana wanapofikia uamuzi wa siri wa kutilikiana na wapenzi wao na kubadili makazi bila kuujulisha upande wa pili.

Kumbe basi, Sauti kama mhusika ameibua dhamira ya athari hasi na changamoto ya teknolojia ya mawasiliano na habari kwa jamii hasa vijana – wanafunzi. Teknolojia hii isipotumika vizuri, huchangia machungu na hasara kwa watu mathalani wanafunzi ambayo huwagharimu wao wenyewe lakini pia taifa (Boumosleh na Jaalouk, 2017; Hossain, 2019; Tangmunkongvorakul, na wenzake, 2019). Kwa mujibu wa ripoti ya robo mwaka (Januari – Machi, 2019) kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communication Regulatory Authority - TCRA), matumizi ya simu kwa ajili ya kupashana habari mionganoni mwa watumiaji yanazidi kuongezeka kila kukicha huku wamiliki wa simu nao wanaongezeka. Kwa hali hii ya ongezeko la watumiaji na wamiliki wa simu, kwa faida ya afya na ustawi wa jamii lazima kutolewe elimu na tahadhari ya kiwango cha juu ili watu wawe na kiasi, subira, umakini na njia mbadala ya kuwasiliana ili kuepuka athari hasi.

Alichokifanya Joan ni mojawapo ya madhara hasi ya matumizi ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Ndiyo maana, Carol Dickson-Carr (2005) anatukumbusha kwa kusema “Remember that in the extreme, communication breakdown can cost you relationships and in business can also cost you money.” (*kumbuka katika kutokuwa na kiasi, tatizo la mawasiliano linaweza kuharibu (kuyagharimu) mahusiano yako pia katika biashara linaweza kusababisha upate hasara - kifedha (Tafsiri ni yangu mwandishi).*).

Umuhimu wa Kufanya Tathmini Kabla ya Kuamua Jambo

Tathmini ni “*angalia kitu kwa undani kisha kadiria bei au ubora wake*” (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, ktj.). Kwa muktadha wa makala haya, tathmini itarejelea mchakato wa kuchunguza jambo kwa kina ili kubaini kufaa na kutokufaa kwake ili uweze kufanya uamuzi sahihi usiokuwa na majuto. Tathmini husaidia kujenga daraja imara kati ya mabunio na uhalisi. Watu wasiopenda kufanya tathmini, daima hujikuta wakifanya maamuzi ya kukurupuka ambayo mwishoni huleta majuto na misiba. Katika maisha hatupaswi kukurupuka kufanya maamuzi hususani tunapojikuta tupo katikati ya wimbi la mawazo yanayoibua nadharia tete. Utulivu, mantiki na fikra ni muhimu sana katika kila pito tunalolipitia hapa duniani. Dhamira hii imeibuliwa na mhusika Sauti kama tunavyothibitisha;

Sauti: Mpenzi wako Alex. Unaendeleaje Waridi wangu?

Joan: (*Anapigwa na butwaa, haamini anachokisikia, anapumua kwa nguvu, anapiga moyo konde, anajaribu kuficha masaibu yake, kisha anajibu*).

Mhuu...! Wow...! Alex my love, uko wapi mpenzi? Nimekukumbuka sana

Alex: Mhh...! Mbona umepumua hivyo? Nisamehe Waridi wangu, nilipata matatizo makubwa na kupoteza mawasiliano. Leo ndo nimebahatika kuipata namba yako. Vipi kichanga chetu ndo kinakutia hasira hivyo. Hicho lazima kiwe kidume. Nipo njiani nakuja Dar kuwaona wapenzi wangu.

Joan: Mhuuu...! (*anashusha pumzi kwa nguvu kisha anakata simu*). Kumbe ninamfikiria Alex wa watu vibaya tu, hivi akija nitamwambia nini kuhusu damu yake? Sipo tayari kuyasema haya kwa kinywa changu. Laiti kama ningalimsikiliza Mary..., hakika Sikitu ameniingiza choo cha kiume! (*anawaza*) Aha, halafu leo Shangazi Linda na mama waliahidi kunipigia simu, nasikitika kwa kuwa hawatanipata, ngoja niharakishe (*anaendelea kuwaza*). (uk. 75 - 76)

Nukuu hii inaonesha ya kwamba, Joan baada ya kugundua kuwa sauti anayoisikia ni ya mpenzi wake, ilhali alishachukua uamuzi wa kuua kiumbe, baada ya kutokumpata hewani Alex kwa kipindi kirefu, anajikuta akijutia uamuzi huo alioutekeleza kwa kudhania ya kwamba mpenzi wake (Alex) alikuwa amemkimbia na kumtelekeza baada ya kumpa ujauzito na bila shaka atakuwa amepata mwanamke mwengine. Joan anasema;

Joan: (*Anajishika kiuno, kwa ujasiri anasema*) Mary, wewe ni rafiki yangu wa moyo, siwezi kukuficha kitu. Lengo la kukuita hapa ni ili unisidie niende nikaitoe hii mimba.

Mary: (*Anasimama ghafla*) Etiii...! No, I can not do such a mistake my friend. That is killing the innocent baby.

Joan: Kwa hiyo umenigomea?

Mary: Sio kukugomea lakini siwezi kukuruhusu ukafanya hilo. Umeanza lini kuwa muuaji Joan?

Joan: Mimi nitaleaje hii mimba wakati kijana mwenyewe hata simpati kwenye simu? Nikijifungua nani atanisaidia? Wazazi wangu watanielewaje? (uk. 49)

Joan: (*Anamkazia Mary macho*). We unachukulia poa sio. Maisha si mchezo Mary. Alex mwenyewe ukute kapata mwanamke mwengine.

Mary: Mwanaume anayeweza kukoaa si Alex peke yake. Isitoshe Alex sio mwanaume wa kuchezea wasichana, ninaamini kabisa kuwa kuna kitu kimempata, sio bure (*anamtazama Joan kwa jicho la ukali*).

Joan: Mie nimeshaamua Mary, huwezi kunibadilisha msimamo wangu (*anakunja ndita na kumjibu Mary kwa hasira*). (uk. 50)

Majadiliano haya yanaonesha ya kwamba Joan alikuwa ameibua nadharia tete juu ya mpenzi wake, Alex lakini pasipo kufanya tathmini ya kina, tena ya kisayansi, akaamua kufanya maamuzi ambayo yalikuwa siyo sahihi. Uamuza huu hatimaye ulisababisha yeze kujiua kwani alikosa ujasiri wa kuja kumkabili Alex. Hapa tunaona namna Mhusika Sauti anavyotukumbusha umuhimu wa kufanya uchunguzi wa kina kabla ya kuchukua uamuzi mgumu ili kuepuwa athari hasi kama ilivyotokea kwa Joan baada ya Alex kumpigia simu na kumueleza yaliyomkuta, wapi alipo kwa sasa na nini anachokitaraja kwa Joan. Laiti Joan angekuwa mtulivu wa mantiki na fikra, bila shaka angepata muda wa kutafakari na kuzitathmini nadharia tete juu ya maisha yake na Alex. Kipeperushi chenye kichwa kisemacho, “*Assessing the situation and choosing priority actions*” kinaonesha ya kwamba, watu wasiokuwa na utamaduni wa kuheshimu sheria wala kujitathmini wako katika hatari kubwa ya kuangamia katika nyanja na njia mbalimbali maishani. Ndiyo maana Femina Hip (2017) wanawahamasisha vijana kujihadhari na maisha ya kuiga, kutokujijali, kutotafiti au kuficha mambo yanayoweza kuhatarisha thamani na hatima ya maisha yao.

Haya yote yametokea baada ya jamii nydingi za zama hizi kuua mfumo wa maisha ya jamii kuwa familia moja pana inayotangamana vema. Kwa sababu, kwa mfumo wa jamii ya familia moja pana, lazima Joan angewafahamu ndugu, jamaa na marafiki wa Alex. Hivyo angeweza kuwasiliana nao, na kupitia wao angempata Alex; vivyo hivyo kwa Alex kwa ndugu na marafiki wa Joan. Ujana usiozingatia mila na desturi za kujitunza na kuheshimu maumbile yako mwenyewe mpaka pale utakapoingia kwenye ndoa, ndiyo chanzo cha yote yaliyomfika Joan. Kwa kutokufanya tathmini ya kisayansi, na kuua mfumo wa jamii kama familia pana, Joan amejikuta akiishia kujilaumu baada ya kugundua mabunio ya Mary yalikuwa sahihi tofauti na mabunio na mahitimisho aliyyoyazalisha yeze kama alivyokiri mwenyewe, “*Kumbe ninamfikiria Alex wa watu vibaya tu, hivi akija nitamwambia nini kuhusu damu yake? Sipo tayari kuyasema haya kwa kinywa changu. Laiti kama ningalimsikiliza Mary [...].*” Hatimaye Joan akajiua na kuacha ujumbe, ambao sehemu yake inasomeka, “[...] Nimekosa amani mimi, nikilala mzimu wa mama yangu na kichanga nilichokiua hunililia sana... Naomba mnisamehe na mniombee msamaha kwa Mungu. Mimi Joan, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu ye yeyote nimeamua kuutoa uhai wangu leo tarehe 29/05/2019 kwa kunywa sumu.”

HITIMISHO

Kwa hakika, utunzi siyo mchakato wa kukurupuka bali kutulia na kulisana wazo vilivyo kwa msaada wa fani iliyofumwa ikafumika. Waandishi Eric F. Ndumbaro na Maria N. Isaya, wametambua thamani ya kuwa na mhusika dhahania na kumpa wajibu mzito wa kumchachafya Joan kama sehemu ya adhabu ya kumrudisha katika adili na tenzi. Waandishi wameitendea haki falsafa ya Kiafrika kwa kiwango cha juu. Tofauti na matarajio ya mhusika Sauti, adhabu hii ya kusutwa kikorasi imeonekana kuwa ni kubwa kuliko adhabu ya kupigwa ngumi, vibao au viboko. Matokeo yake badala ya kuponya moyo uliojeruhika kwa kuparamia ya dunia, jamii ya waadilifu imeishia kumsukuma na kumzodoo Joan hadi akaona heri kujiua kuliko kuendelea kubebewa kibwebwe na kigodoro. Tunachojifunza hapa, ni kwamba, kila mmoja wetu ana

wajibu wa kutunza uumbaji wa Mungu – uwe uumbaji uliokengeuka au usiokuwa na mawaa; yote tuitunze.

Tamthilia hii ni ya kitanzia ambayo binti mnyonge na tegemeo la familia anakatishwa ndoto zake kutokana na kujiingiza katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia ya mawasiliano, pia ulimwengu wa mahusiano ya kimapenzi pasipo kuwa na elimu sahihi ya mahusiano na ujauzito pamoja na kutokuwa na hofu ya Mungu. Kumbe basi, tamthilia hii mbali na fasihi, uhakiki na nadharia, inaweza kutumika pia kufundisha masomo au kozi za *guidance and counseling, psychotherapy, general psychology*, kutaja kozi chache. Pia, tamthilia hii inafaa kutumika kama darasa la msaada kwa jamii nzima, watungaji na wasimamizi wa sera kubadili msimamo, mtizamo na mbinu za kupambana na ukengeushi wa wanafunzi hasa watoto wa kike shulen ni vyuoni.

MAREJEO

- Assessing the situation and choosing priority actions.
<https://www.who.int/roadsafety/projects/manuals/alcohol/2-Assessing.pdf>.
- Bertонcini, E. Z. (1989). *Outline of Swahili literature*. Leiden: E. J. Brill.
- Bible Society of Tanzania. (1997). *Maandiko Matakatifu ya Mungu Yaitwayo BIBLIA*. Nairobi: Africa Area Typesetting Unit.
- Boumosleh, J. na Jaalouk, D. (2017). Smartphone Addiction among University Students and Its Relationship with Academic Performance. In *Global Journal of Health Science* (Vol. 10, No. 1; 2018).
https://www.researchgate.net/publication/321165231_Smartphone_Addiction_among_University_Students_and_Its_Relationship_with_Academic_Performance/download
- Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara. (Januari, 2016). *Mtoto na Haki Zake: Sheria katika Lugha Rahisi*. <https://tls.or.tz/publication/view/ijue-sheria-ya-mtoto-na-haki-zake/>
- DHS programme. (2010). *Atlas ya Afya ya Mama, Afya ya Mtoto na Liske, Tanzania*.
<https://dhsprogram.com/pubs/pdf/ATR11/ATR11.pdf>
- Dickson-Carr, C. (2005). Strategies to Overcoming Communication Breakdown. Power-Ed Solutions, Inc.
<http://managingpersonalresources.com/ComunicationStrategies.pdf>.
- Femina Hip. (2017). *Linda Maisha Yako*.
http://www.feminahip.or.tz/fileadmin/03_downloads/03_magazines/03_others/GirlPowerSRHR2017.pdf
- Hossain, M. (2019). Impact of Mobile Phone Usage on Academic Performance. In *World Scientific News: an international scientific journal* (WSN 118, 164 - 180).
https://www.researchgate.net/publication/330410485_Impact_of_Mobile_Phone_Usage_on_Academic_Performance/link/5c3ead4b92851c22a378679c/download.
- https://www.bbc.com/swahili/habari/2012/01/120119_abortion
- International Criminal Court. (Novemba, 2016). *Sera ya Watoto*. <https://www.icccpi.int/iccdocs/otp/20161115 OTP ICC Policy-on-Children Swa.PDF>
- International Youth Foundation. (Hakuna mwaka). Mafunzo ya Afya ya Uzazi: Nyongeza ya Mtalaal kwa Vijana Umeigwa kwa Mtindo wa Kenya.
https://www.iyfnet.org/sites/default/files/P4L_Supplement_Kenya_Kiswa.pdf

- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2000). *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977*. Dar es Salaam: Mpigachapa wa Serikali.
- Joseph na Bontrager, G. (2014). *Maisha ya Uzima*. <http://equip4change.org/pdf/swahili/level2/Maisha-ya-Uzima.pdf>.
- Kituo cha Ushauri Nasaha, Liske na Afya (COUNSENUTH) na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. (2015). *Ijue Haki Mpya za Uzazi: Katika Sheria Mpya ya Kazi Tanzania*. <http://counsenuth-tz.org/wp-content/uploads/2017/10/Zijue-Haki-za-Uzazi-katika-Sheria-Mpya-ya-Kazi-Tanzania.pdf>
- Lynch, P. A. na Roberts, J. (2010). *African Mythology A to Z* (second edition). <https://img.fireden.net/tg/image/1454/78/1454787608049.pdf>
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: nadharia, historia na misini ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd na Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religion and Philosophy*. London: Morrison and Gbb Ltd.
- Mohamed, S. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Motte, J. (Hakuna mwaka). Uhusiano wa hali ya hewa na maisha ya kiroho. https://www.vemission.org/fileadmin/redakteure/Dokumente/JPIC/Climate_and_s_piri_kisuaheli.pdf
- Mulokozi, M. M. (2017). *Taaluma ya Lugha na Fasihi - 2: Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es salaam: KAUTTU.
- Mung'ong'o, C. G. (1977). *Mirathi ya Hatari*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Mwongozo wa Stadi za Mpango wa Maisha Tanzania. Stadi za Mpango wa Maisha Mtaala wa Vijana wa Afrika: Toleo la Tanzania. https://path.azureedge.net/media/documents/HIV-TB_aya_lps_facilitator_tanz_ki_sec3.pdf
- Ndumbaro, E. F. na Isaya, M. N. (2019). *Usinie*.
- Njogu, K., na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: nadharia na mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- p'Bitek, O. (1975). *Wimbo wa Lawino: ombolezo*. Dar es salaam: EAPH
- Ruhumbika, G. (2002). *Janga Sugu la Wazawa*. Dar es salaam: E & D Vision Publishing.
- Rumanyika, J. (2016). Contemporary Challenges Facing Mobile Networks Operators: A Comparative Survey Reflecting Migration from 3rd Generation to 4th Generation of Mobile Communications between Tanzania and other Parts of the World. In *International Journal of Engineering Works* (Vol. 3, Issue 3, PP. 6-18). https://www.researchgate.net/publication/301899201_Contemporary_Challenges_Facing_Mobile_Networks_Operators_A_Comparative_Survey_Reflecting_Migration_from_3rd_Generation_to_4th_Generation_of_Mobile_Communications_Between_Tanzania_and_other_Parts_of_th/link/572c641908ae25c48c308a2b/download
- Salem, H. S. (Mh.) na UN Environment (2019). Global Environment Outlook – GEO-6: Healthy Planet, Healthy People. Cambridge: University Printing House. https://www.researchgate.net/publication/331832227_UN_Environment_2019_Global_Environment_Outlook_-_GEO-6_Healthy_Planet_Healthy_People_Nairobi_Kenya_University_Printing_House_Cambridge_UK_Hilmi_S_Salem_External_ReviewerEditor_Also_mentioned_and_cited/link/5c92989ca6fdcccd4602e18d4/download
- Semzaba, E. (2008). *Marimba ya Majaliwa*. Dar es salaam: E & D Vision Publishing.
- Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es salaam: Press and Publicity Centre

- Senkoro, F. E. M. K. (1995). E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili. Katika *Kioo cha Lugha* (Juzuu 1, Na. 1). <https://www.google.com/search?client=firefox-b-d&q=kezilahabi+ni+nani+by+senkoro>.
- Tangmunkongvorakul, A., na wenzake (2019). Association of excessive smartphone use with psychological well-being among university students in Chiang Mai, Thailand. In *PLOS ONE*. <https://journals.plos.org/plosone/article?id=10.1371/journal.pone.0210294>
- Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA), Bangladesh Institute of ICT in Development (BIID) and Tanzania Telecentre Network (TTN). (2011). Reaching to Rural (R2R) Connecting the rural Tanzania through Telecentres: report on Joint Impact Assessment, Services Need Analysis and Designing Business Model Towards Developing A Sustainable Network of Telecentres in The United Republic of Tanzania. <https://www.tcra.go.tz/images/documents/reports/telecentresReport.pdf>.
- Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA). (2019). QUARTERLY COMMUNICATIONS STATISTICS: January-March 2019 Operators' Submissions. https://www.tcra.go.tz/images/headlines/TelCom_Statistics_March_2019.pdf
- TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Tumerithi Tuwarithishe. (2016). *Misitu, Utawala bora na Maendeleo ya Taifa: Kutafakari tena Mapendekazo ya Kuboresha Utawala wa Misitu nchini Tanzania Yaliyotolewa na Shirika la TRAFFIC kwenye Ripoti ya Mwaka 2007*. https://www.tnrf.org/files/mmc_policy_brief_swahili_0.pdf
- United Nations Environment Programme. (2018). Adaptation Gap Reports. https://wedocs.unep.org/bitstream/handle/20.500.11822/27114/AGR_2018.pdf?sequence=3.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi* (chapa ya tano). Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wazambi, F. na Mikongoti, P. (2018). Muhtasari wa Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania 2017: Tanzania Bara. Dares salaam: Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. [https://humanrights.or.tz/assets/images/upload/files/THRR%202017%20Swahili%20Booklet%20\(1\).pdf](https://humanrights.or.tz/assets/images/upload/files/THRR%202017%20Swahili%20Booklet%20(1).pdf)